**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Nafasi ya Ikolojia ya Lugha katika Mtagusano wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Dini katika Kaunti ya Bungoma

*Martin Barasa Mulwale[1*], Prof. Florence Ngesa Indede, PhD[1] na Dkt. Beverlyne Asiko Ambuyo, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu Kishirikishi cha Maseno, S. L. P. 333, Maseno, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0002-9871-4647; Barua pepe ya mawasiliano: mulwalemartin@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*27 Machi 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Ikolojia, Mawanda ya Dini, Wingilugha, Ubadilishaji, Uchanganyaji Msimbo.*

**IKISIRI**

Nyanja mbalimbali katika jamii hutegemea matumizi ya lugha. Hali hii huzua changamoto ya namna ya kutumia raslimali za lugha zinazopatikana katika jamiilugha fulani. Juhudi ya kufahamu na kutagusana na ulimwengu huhitaji matumizi ya kiisimu ya kipekee. Katika muktadha wa kidini kuna changamoto ya asili ya maneno, mamlaka, utambulisho na ushirikiano wa wahusika. Aidha, miktadha mbalimbali ya kidini hutumia lugha kutimiza mahitaji yake maalum. Lugha hutenda matendo, huomba maombi ya kukemea, husimulia hali za kijamii na hata huonekana kudhibiti matendo ya Maulana. Ni kwa misingi hii ndipo kazi hii inajukumika kutalii jinsi lugha ya Kiswahili na Kibukusu zinavyotagusana katika mawanda haya ya dini, hasa Dini ya Musambwa (DYM) ambayo inaaminika kuwa ya kiasili katika jamii hii ya Wabukusu katika Kaunti ya Bungoma. Kazi hii inazingatia misingi ya Spolsky (2004, 2006, 2009) ambaye anajadili kuwa sera ya lugha halisi ya jamii hupatikana kwenye matumizi yake. Anazingatia Mwelekeo wa ikolojia ya lugha uliozinduliwa na Haugen (1972) unaochunguza mwingiliano baina ya lugha na mazingira. Muundo wa kiuchanganuzi ulitumiwa. Kupitia uchunzaji wa kutoshiriki moja kwa moja mtafiti alihudhuria ibada na kunasa mazungumzo yao kwenye kanda ya kunasia sauti. Mazungumzo hayo yalinakiliwa na orodha ya uchunzaji ilitumiwa kubainisha na kueleza namna lugha ya Kibukusu na Kiswahili zilivyotumiwa katika shughuli za kanisa hilo. Hali ya kuchanganya na kubadili msimbo, utohozi na hata matumizi ya Kiswahili kwa Kibukusu haikuweza kuepukika. Utafiti huu unadhihirisha kuwa raslimali za lugha zilizopo katika ikolojia fulani huchagizana katika kukamilisha majukumu ya mawasiliano katika muktadha husika.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

**APA CITATION**

Mulwale, B. M., Indede, F. N. & Ambuyo, B. A. (2023). Nafasi ya Ikolojia ya Lugha katika Mtagusano wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Dini katika Kaunti ya Bungoma *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 23-39. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147.

**CHICAGO CITATION**

Mulwale, Martin Barasa, Florence Ngesa Indede and Beverlyne Asiko Ambuyo. 2023. "Nafasi ya Ikolojia ya Lugha katika Mtagusano wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Dini katika Kaunti ya Bungoma". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 23-39. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147.

**HARVARD CITATION**

Mulwale, B. M., Indede, F. N. & Ambuyo, B. A. (2023) "Nafasi ya Ikolojia ya Lugha katika Mtagusano wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Dini katika Kaunti ya Bungoma", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 23-39. doi: 10.37284/jammk.6.1.1147.

**IEEE CITATION**

B. M. Mulwale, F. N. Indede & B. A. Ambuyo, "Nafasi ya Ikolojia ya Lugha katika Mtagusano wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Dini katika Kaunti ya Bungoma", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 23-39, Mar. 2023.

**MLA CITATION**

Mulwale, Martin Barasa, Florence Ngesa Indede & Beverlyne Asiko Ambuyo. "Nafasi ya Ikolojia ya Lugha katika Mtagusano wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Dini katika Kaunti ya Bungoma". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Mar. 2023, pp. 23-39, doi:10.37284/jammk.6.1.1147.

## UTANGULIZI

Lugha ni zana ya kutimiza majukumu mbalimbali ya kibinadamu. Juhudi nyingi za kujenga taifa lenye maendeleo na kubuni kazi haziwezi kufua dafu bila kushirikisha ajenda ya lugha (Shitemi, 2011). Nyanja mbalimbali hutegemea matumizi ya lugha kama vile maendeleo ya kiuchumi, uajiri, sheria, ulinzi, mshikamano wa kijamii na mitagusano ya kitamaduni. Hali hii huzua changamoto ya namna ya kutumia raslimali za lugha zinazopatikana katika jamiilugha fulani. Juhudi ya kufahamu na kutagusana na ulimwengu huhitaji matumizi ya kiisimu ya kipekee. Katika muktadha wa kidini kuna changamoto ya asili ya maneno, mamlaka, utambulisho na hata ushirikiano wa wahusika. Miktadha mbalimbali ya kidini hutumia lugha kutimiza mahitaji yake. William (1992) anajadili kuwa wanaisimu jamii huchunguza lugha wakiihusisha na uhalisia uliopo. Hivi kwamba dini ni mawanda mojawapo inayohusu tabia za binadamu ambapo uamilifu wa lugha ni muhimu. Anaendelea kusema kuwa lugha hutimiza malengo maalum kwa namna inavyotumiwa. Lugha hutenda matendo, huomba maombi ya kukemea, husimulia hali za kijamii, huonekana kudhibiti matendo ya Maulana na kadhalika. Haya yanaoana na maoni ya Halliday (1994) ya uamilifu wa lugha katika miktadha tofauti tofauti. Ni kwa misingi hii ndipo kazi hii inajukumika kutalii jinsi lugha ya Kiswahili na Kibukusu zinavyotagusana katika mawanda haya ya dini, hasa Dini ya Musambwa (DYM) ambayo inaaminika kuwa ya kiasili katika jamii hii ya Wabukusu katika Kaunti ya Bungoma.

### Nafasi ya Lugha ya Kiswahili na Kibukusu katika Kaunti ya Bungoma

Kiswahili ndiyo lugha ya taifa nchini Kenya na kwa kiasi kikubwa inaeleweka na kutumiwa na wakenya wengi kwa ajili ya mawasiliano ya kila siku. Katiba ya Kenya (2010) inatambua lugha hii kama lugha ya kitaifa na vilevile lugha rasmi. Hii ina maana kuwa lugha hii imepewa majukumu kimatumizi kwa njia rasmi tofauti na ilivyokuwa awali. Kiswahili kilichukuliwa kuwa lugha ya watu duni na wale wasio na elimu ya kisasa hali ambayo imebadilika kulingana na hadhi ya lugha hii katika jamii hivi sasa. Aidha, lugha hii inatambulika kama lugha mojawapo rasmi ya jumuiya ya Afrika Mashariki na kupendekezwa kuwa lugha ya Muungano wa Afrika. Ni dhahiri kwamba lugha hii inatumiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii ; biashara, elimu, dini, siasa na hata mitagusano ya kijamii.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

Kama lugha ya taifa inaendeleza majukumu ya kuwaleta watu wa jamii mbalimbali, ambao lugha zao za mama hutofautiana pamoja katika shughuli za kitaifa.

Kaunti ya Bungoma ni kielelezo cha changamoto ambazo ni dhahiri, na zinazoakisi namna utekelezwaji wa mfumo mpya wa ugatuzi nchini Kenya unavyotarajiwa kukabiliana na mitazamo ya kijamii inayodhihirisha upendeleo wa lugha fulani kutokana na dhima yake, huku mingine ikidhihirisha kauli kuwa watu hujieleza vyema katika lugha zao za kiasili (UNESCO, 2003). Kulingana na Batibo (2005), mataifa mengi barani Afrika yana mpangilio wa traiglosia ambapo lugha za kikoloni ndizo zenye hadhi ya juu na hutekeleza majukumu rasmi, lugha za kieneo ambazo ni za kimtagusano baina ya makundi mbalimbali ya kijamii na lugha asili ambazo hutekeleza majukumu ya hadhi ya chini. Katika Kaunti ya Bungoma, hali inayojitokeza ni mifumo miwili ya ujozi lugha na daiglosia ambapo Kiswahili na Kibukusu zinashindana. Kulingana na Sebba (2011), hali ya ujozi lugha unaoenda sambamba na daiglosia husababisha hali lugha husika kutumika lakini zikiwa zimetenganishwa kutegemea majukumu zinazotekeleza. Hali hii inasheheni ugiligili wa kiutendeti na wa kimtazamo unaodhihirisha uegemezi wa kimatumizi kwa upande wa Kiswahili ikilinganishwa na Kibukusu.

Hata hivyo, msimamo wa kikatiba kuhusu lugha ni fursa kwa wadau wote katika ngazi za kijamii kutambua Kiswahili na Kibukusu kama kiungo muhimu cha kuimarisha na kudumisha usimamizi bora katika asasi mbalimbali za serikali na za umma, kwa vile hii ni hatua muhimu inayofanikisha viwango vya ubora katika ugavi wa rasilimali za kimsingi na huduma muhimu. Aidha, pana haja ya kuzindua nyenzo za kuzipa lugha za kiasili hususan Kibukusu msukumo wa ‘kimatumizi’ kupitia miktadha rasmi na ya kijamii (Brenzinger, 2007), ili kiweze kutimiza majukumu yake ya kimawasiliano katika kiwango cha Kaunti hasa maeneo ya mashinani, na ambayo yanazidi kunyakuliwa na Kiswahili; na namna ambavyo Kibukusu kinaweza kukabiliana na nguvu dukizi zinazotokana na kuidhinishwa kikatiba kwa Kiswahili lugha rasmi nchini Kenya.

**Dini ya Msambwa (DYM)**

Kuloba (2014) anaeleza kuwa Dini ya Musambwa ni mojawapo ya dini ya kiasili Afrika Mashariki. Mwanzilishi wake ni Bw. Elijah Masinde miaka ya 1940 kutokana na kupinga kwa utawala wa mkoloni na Ukristo wa wamishonari nchini Kenya. Anaendelea kusema kuwa ingawa DYM sio kanisa la Kikristo, misingi ya mafunzo yake ni Agano la kale kwenye Biblia takatifu. Dini hii inaweza kuelezwa kuwa imeundwa kwa mseto wa idiolojia za utamaduni wa Kiafrika na Biblia. Dini hii ilisisitiza hali ya urejesho wa watu kwa mizizi au tamaduni za mababu wa kale (Msambwa). Mungu wao ambaye alijulikana kama *Wele* angemtumia Masia kuwaongoza Waafrika ili warudi kwenye tamaduni zao. Hali ngumu ya kimazingira iliyoendelezwa na mkoloni ilimfanya Mwafrika kutaka kujinasibisha zaidi na asili yake. Wafuasi wengi wa dini hii wapo katika Kaunti ya Bungoma na Trans Nzoia ila kunao wachache katika maeneo ya Mbale, Manafwa na Bududa kule Uganda.

Kutokana na chimbuko hili la DYM, inatazamiwa kuwa lugha ya Kibukusu ambayo ndiyo lugha ya kiasili ndiyo inayotumiwa kuendeleza shughuli za dhehebu hili. Ugiligili unatokea pale ambapo sasa lugha ya Kiswahili pia ni muhimu katika kuendeleza utaifa nchini. Hali hii husababisha lugha hizi kuweza kutumika kwa namna fulani katika mazingira haya ili kutimiza majukumu yake katika mawanda haya ya dini. Kazi hii inatathmini namna lugha hizi kutagusana na kukamilishana katika kufanikisha shughuli za dini hii kama vile mahubiri, maombi, ubatizo, maelekezi na ufahamishaji wa miradi mbalimbali katika kanisa na shughuli nyinginezo.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

**Swala la Utafiti**

Umuhimu wa dini kama mawanda mojawapo ya kuchunguza aina mbalimbali za lugha, mabadiliko, udumishaji, sera na mipango ya lugha katika jamii ni sehemu inayotambulika katika baadhi ya kazi za mwanzomwanzo za wanaisimu mbalimbali. Aidha, kazi nyinginezo pia zilichunguza nafasi ya wamishonari katika matumizi, maenezi, usanifishaji na masuala ya ikolojia ya lugha kwa jumla. Hii ni ithibati ya uhusiano uliopo kati ya lugha na shughuli za kidini. Lugha hutumiwa kusababisha matendo na hali fulani za kidini kutokea, hivyo basi katika jamii ya wingilugha, changamoto ya namna ya kutumia lugha hizi huibuka. Kazi hii inachunguza namna lugha ya Kibukusu na Kiswahili zinatumika katika mazingira yasiyoshurutisha ni lugha ipi itumike wapi na kwa minajili gani katika mawanda ya DYM katika Kaunti ya Bungoma.

**Madhumuni**

Malengo ya kazi hii ni kutathmini nafasi ya lugha ya Kiswahili na Kibukusu katika kukamilisha shughuli mbalimbali zinazoendeshwa katika dhehebu la DYM.

**NADHARIA YA UTAFITI**

Spolsky (2004, 2006, 2009) anafafanua kuwa sera ya lugha halisi ya jamii hupatikana kwenye usimamizi wake. Anatumia mihimili mitatu kueleza sera ya lugha ambayo ni usimamizi wa lugha, ikolojia ya lugha na idiolojia ya lugha. Hivyo basi, matumizi yake namna yanavyoelezwa kwenye sheria kama vile katiba za nchi haidhihirishi hali halisi ya lugha. Ni muhimu kutambua kuwa baadhi ya lugha huonekana kuenea zaidi kutokana na sababu mbalimbali za uamilifu wake katika jamii. Lugha hupata utambulisho wake kwa namna inavyotumiwa katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Kazi hii inazingatia mwelekeo wa ikolojia ya lugha.

**Ikolojia ya Lugha**

Mwelekeo wa ikolojia ya lugha ulizinduliwa na Haugen (1972), na umefasiliwa kama uchunguzi kuhusu mwingiliano baina ya lugha na mazingira. Kanuni ya kimsingi ya dhana ya ikolojia ya lugha kwa mujibu wa Haugen ni kwamba, lugha hutegemea mazingira inamotumika, na huhifadhiwa akilini mwa watumiaji wa lugha husika. Kwa vile lugha ni kiungo muhimu kinachowaweka pamoja watumiaji lugha husika, mazingira ya kijamii na yale halisi yana umuhimu mkubwa katika kuelekeza mkondo wa matumizi ya lugha katika jamii husika. Kwa mujibu wa Martin (2007), mtagusano kati ya lugha na mazingira zinakozungumzwa lugha hizo hudhihirisha uhusiano wa kutegemeana. Uhusiano huu hutambulika kupitia mifumo ya kijamii inayoambatana na miktadha halisi ya kijamii, kisiasa na kihistoria ambamo lugha hutumika. Kulingana na Skutnabb-Kangas na Harmon (2018), mazingira halisi ni kigezo cha kimsingi kinachobaini uhusiano dhahiri uliopo baina ya lugha mbalimbali na wazungumzaji wa lugha hizo.

Dhana ya Ikolojia ya Lugha vilevile inakariri kuhusu dhima ya utambuzi kuhusu uhai wa lugha, malengo pamoja na miundo yake kama msingi wa ukuzaji, udumishaji na uhifadhi wa lugha (Bastardas-Boada, 2002). Dhana hii inapambanua jinsi lugha zinavyozuka na kutagusana katika mfumo hai na ambao unadhihirisha kanuni za mtagusano wa lugha katika miktadha ya kijamii, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi.

Kaplan na Baldauf (1997), wametumia mtazamo huu katika kuchanganua masuala yanayohusu sera na upangaji lugha ambapo wanahoji kuwa, upangaji lugha haupasi kuzuiliwa katika uimarishaji wa lugha moja na kutupilia mbali lugha zingine ambazo zinatumika katika mazingira sawa. Mtazamo wao unaakisi nguvu tekelezi katika ikolojia ya kiisimu, kwa vile wanatilia mkazo vipengele vyote vya michakato ya lugha kama vile; kutoweka kwa lugha, juhudi za udumishaji na ufufuaji wa lugha, mbanduko na maenezi ya lugha, wiano na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

mtagusano wa lugha, ukuaji wa pijini na krioli na matumizi ya lugha katika mfumo maalum wa kisanii. Kwa mujibu wa Baker (2001), dhana hii inadadavua maswala yanayohusu ustawishaji na udumishaji wa lugha, na kitovu chake cha uchanganuzi wake ni mwingiliano wa lugha mbalimbali katika mazingira halisi.

Tafiti za Auburger (1990), Phillipson na Skutnabb-Kangas (1996), na Ricento (2000) zimeangazia kwa kina suala la kudhoofika kwa lugha kama kipengee mojawapo cha ikolojia ya lugha. Hali hii imepata msukumo kutokana na udhibiti wa Kiingereza kote ulimwenguni ambapo kumekuwa na shinikizo katika viwango mbalimbali vya asasi za utawala zinazochangia katika kuwepo kwa 'umoja lugha' kama ishara ya usasaishaji na umataifishaji wa lugha kwa upande mmoja, huku kukiwa na jitihada chungu nzima zinazowania kuendeleza wingi lugha kama haki ya kimsingi na ya kibinadamu kwa upande mwingine. Wao wanatambua namna ambavyo ulowezi wa kiisimu unavyodumisha udhibiti wa lugha kama njia mojawapo ya kukabiliana na tukio la wingi lugha. Huku Van Lier (2000) akishikilia kuwa mtazamo wa kiikolojia ni hatua muhimu katika maendeleo ya lugha, hususan ujifunzaji na uamilifu wa lugha, Barron na wenzake (2002), wameeleza dhana ya ikolojia ya lugha kwa kuangazia jinsi wanajamii wanavyoimudu lugha kupitia katika mawanda mbalimbali ya kimatumizi.

Ferguson (1959) anabainisha kuwa muktadha wa dayaglosia huwasilisha hali kuwa lugha fulani huonekana kuwa ya hadhi ya juu au chini kutegemea mawanda inamotumika. Anaonyesha kwa mfano namna miktadha kama vile ya mahubiri ya kidini, mihadhara ya vyuo vikuu au magazeti ingetumia lugha ya hadhi ya juu ilhali mazungumzo ya kawaida katika familia au kati ya marafiki ingetumia ile ya hadhi ya chini. Mtazamo huu unatathmini jinsi hali hii inavyochangia katika kudhoofika au kuimarika kwa Kiswahili na Kibukusu kiuamilifu katika mazingira yenye wingi lugha. Kwa minajili ya kazi hii mawanda yatakayoshughulikiwa ni dini, ni kwa namna gani lugha ya Kiswahili na Kibukusu zinavyotagusana na kukamilishana katika kuendeleza au kustawisha mawasiliano.

Province na Kretzer (2018) wanaeleza kuwa kipengele cha Ikolojia ya Lugha huhusu maamuzi ya uchaguzi wote wa kiisimu ambao hufanywa na watu au kundi la watu. Kutokana na msingi huu, dhana ya ikolojia ya lugha ni uchunguzi wa kimseto katika miktadha maalum ya kijamii na kisiasa, ambapo hali mbalimbali kuhusu lugha hubuni, huakisi na huchambua mifumo na mamlaka mbalimbali. Mitazamo kuhusu ikolojia ya lugha imeelekeza utafiti huu kuchanganua mtagusano wa lugha na athari zake katika mawanda ya dini (DYM) katika Kaunti ya Bungoma. Masuala ya uchanganyaji na ubadilishaji wa msimbo kati ya Kiswahili na Kibukusu yatachanganuliwa na kuelezwa namna yanavyotokea katika katika mawanda ya DYM ili kutekeleza au kufanikisha majukumu mbalimbali.

Vandenbussche na Darquennes (2011) wanaeleza kuwa umuhimu wa dini kama mawanda mojawapo ya kuchunguza aina mbalimbali za lugha, mabadiliko, udumishaji, sera na mipango ya lugha katika jamii ni sehemu inayotambulika katika baadhi ya kazi za mwanzomwanzo za Haugen (1953), Fishman (1966), Stewart (1968), Samarin (1976), Ferguson (1982), Spolsky (2006; 2009) miongoni mwa wengine. Kwa mfano wanaeleza kuwa Haugen anajadili mahusiano ya kidini, utambulisho na mabadiliko ya lugha miongoni mwa watu kutoka Norway wanaoishi Amerika. Kazi ya Fishman inaeleza masuala ya kidini yanayoathiri michakato ya mabadiliko na udumishaji wa lugha katika muktadha wa wahamiaji. Stewart naye alieleza uamilifu wa lugha kwa kufafanua matumizi kumi ya lugha katika muktadha teule wa dini fulani. Aidha, Ferguson alichunguza uhusiano uliopo wa maandishi mbalimbali na maenezi ya lugha ulimwenguni. Anaijenga kazi hii kutokana na kazi zake za awali ambazo zilititilia maanani umuhimu wa nafasi ya dini katika kuchunguza muundo wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

kidiaglossia wa uamilifu wa lugha (Ferguson, 1959) na masuala ya Upangaji lugha (Ferguson, 1968).

Aidha, kazi nyinginezo pia zilichunguza nafasi ya wamishonari katika matumizi, maenezi, usanifishaji na masuala ya ikolojia ya lugha kwa jumla (Kaplan & Baldauf, 1997). Spolsky (2006) anafafanua muundo ambao unaeleza mitazamo ya dini na lugha. Kwanza, anafafanua athari ya dini kwa lugha: Uchaguzi wa lugha, udumishaji pamoja na ukopaji wa lugha. Pili, utangamano wa lugha na dini. Tatu, athari ya lugha kwa dini katika ujenzi wa jamii fulani ya kidini na nne ni masuala ya namna lugha na dini huathiri uelewa wa mambo katika jamii. Kwa namna ambavyo hakuridhika na mitazamo hii Spolsky (2009) katika kitabu chake cha *Language Management* anaeleza uhusiano uliopo kati ya dini na sera ya lugha, ambapo anaeleza masuala maalum yanayohusiana na namna dini huathiri upangaji lugha tofauti na namna lugha na dini huathiri uelewa wa mambo katika jamii.

Rahimi na Hematiyan (2011) wanaeleza kuwa lugha inaweza kutumiwa kama silaha. Ina uwezo wa kudanganya, kusifu, kudunisha, kukejeli na kadhalika. Wanaendelea kusema kuwa mikakati mbalimbali hutumiwa katika lugha ya mawanda ya dini ili kuunda masuala na ukweli fulani. Aidha, katika mawanda haya hadithi na mafumbo kuhusu maovu, siku ya kiama na nguvu za maombi huwasilishwa kupitia lugha ili kusababisha matendo fulani. Baadhi ya mikakati inayojitokeza katika matumizi ya lugha ni;

- Kukumbusha ambapo maneno hutumiwa kuyaeleza mambo yaliyopita ili kuwamakinisha watu.
- Kusifu – matendo ya kusifu huwasilishwa kwa maneno machache
- Kujitolea kwa hali fulani kwa kutumia usemi wa kutenda
- Matumizi ya maneno yanayoadhimisha matukio fulani ya kiasili kwa mfano matumizi ya ‘kwa jina la Yesu mwana wa Mungu’
- Kutumia usemi wa kuomba kwa kuuliza maswali au kuwabariki watu
- Kuwahimiza watu kujiunga na shughuli fulani za kidini
- Usemi wa kutia moyo kwa kusisimua hisia za watu ili watekeleze kitendo fulani
- Athari za hadithi, nyimbo, drama na mashairi ya kidini kwa hisia za watu katika kuwasababisha kutenda matendo fulani yanayohusiana na shughuli za kidini.

Mikakati hii huonekana kujitokeza kwa namna ambavyo lugha ya Kiswahili na Kibukusu hutagusana ili kukamilishana katika shughuli za mawanda ya Dini ya Msambwa. Kazi hii inajadili namna lugha hizi mbili humizaniana katika kuyafanikisha majukumu haya.

**Tahakiki ya Maandishi**

Katika jamii yenye wingilugha, upekee wa uamilifu wa lugha hutokea kwa namna ambavyo jamii hiyo huteua na kutumia lugha kuafikia malengo yake. Aghalabu ubadilishaji msimbo hutokea kati ya watumiaji lugha katika viwango mbalimbali. Haya ni maelezo ya Probyn (2009) ambaye alitambua kuwa sehemu nyingi za Afrika Kusini hutumia lugha ya wakoloni ambayo ni Kiingereza kama lugha ya kufunzia hata kabla wanafunzi hawajajimudu vyema katika matumizi yake. Anaendelea kusema kuwa katika hali ambazo lugha ya mama ya walimu na wanafunzi zinafanana hutokea uvunjaji wa sera ya lugha na matumizi ambapo wao huonekana kutumia mkakati wa kubadilisha msimbo ili kuwezesha malengo mbalimbali ya kijamii na kipedagojia. Utafiti huu unatufahamisha kuwa hali ya kubadilisha msimbo hutekelezeka ili kutimiza malengo fulani na huwezekana tu kutokana na raslimali za lugha

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

ambazo watumiaji wanazo zinazofanana. Hoja hii ni muhimu katika utafiti huu kwani inachukuliwa kuwa raslimali ya lugha iliyoko kati wa wazungumzaji wa Kaunti ya Bungoma ni Kibukusu na Kiswahili. Hivyo basi kwa njia moja au nyingine lugha hizi hufidiana kimatumizi ila kwa hali tofautitofauti kutegemea ruwaza za matini zinazojitokeza katika mawasiliano.

Katika kushughulikia suala la upangaji wa lugha wa kimikro katika muktadha wa ikolojia ya lugha Baldauf (2010) anajadili kuwa dhana ya upangaji wa lugha kwa kawaida huchukuliwa kwa kiwango kikubwa kama suala la kitaifa linalotekelezwa na serikali ili kuathiri au kubadili uamilifu wa lugha katika jamii. Anaeleza kuwa upangaji huo hushughulikia maswala manne; upangaji lugha kulingana na jamii, lugha yenyewe, matumizi katika elimu na hadhi yake. Sera za miundo na uamilifu wa lugha sharti izingatiwe. Sera na upangaji lugha katika kiwango hiki umekithiri katika uwanja huu. Hata hivyo katika miaka ya hivi karibuni, suala la upangaji lugha limechukua mkondo mwingine ambapo muktadha wa kiikolojia umetiliwa maanani sana. Hili limesisitiza mtazamo kuwa shughuli ya upangaji lugha hutokea katika viwango mbalimbali; Kiwango cha makro, meso na mikro. Kwa msingi huu suala lingine linajitokeza kuwa, nani ana uwezo wa kuathiri uamilifu wa lugha katika kiwango cha kimikro? Kiwango hiki cha kimikro kinahusu wenyeji wa lugha fulani ambao wanatangamana na raslimali za lugha walizo nazo katika mazingira yao. Hapo ndipo swala la matumizi ya lugha ya Kibukusu na Kiswahili ipo katika Kaunti ya Bungoma. Hawa wenyeji kwa kuwa wana uhuru wa kutumia lugha hizi mbili, ni vipi ambavyo lugha hizi hutumiwa katika mawanda ya DYM?

Aidha, Baldauf (2010) akieleza dhana ya ubadilishaji na uchanganyaji msimbo, anasema kuwa sio tu namna mbalimbali za matumizi ya lugha bali ni namna ya kuhusisha maumbo ya lugha na uamilifu wake katika utekelezaji wake kijamii. Anasisitiza kuwa utafiti kutoka kwa mwanaisimu na mwanaisimu saikolojia hulenga kuelewa hali ya kubadili msimbo kama mbinu ya kutambulisha isimu na michakato yake. Mitazamo ya kisaikolojia na kijamii kuhusu ubadilishaji na uchanganyaji msimbo imejikita katika kutoa majibu ya kwa nini wazungumzaji hubadilisha msimbo na maana yake au umuhimu wake kijamii. Matokeo yake hutumiwa kueleza namna lugha hufanya kazi kama mchakato wa kijamii. Hili lilielezwa pia na Mabule (2015) ambaye alisisitiza kuwa ubadilishaji msimbo sio ishara ya upungufu wa kiisimu inavyoelezwa na Hamers na Blanc (2000) bali ni hali inayotumiwa na watumiaji wa lugha kuwasilisha maana mbalimbali. Anaendelea kusema kuwa uteuzi wa lugha fulani kati ya wazungumzaji huwajulisha muktadha na mitazamo ya kijamii ambayo mawasiliano fulani yanaelekezwa. Anatambua kuwa lugha nyingi zimekua kutokana na hali ya kukopa misamiati kutoka lugha mbalimbali. Hali hii huchangia katika kuipandisha hadhi ya lugha na kuifanya ikubalike katika maeneo mengi. Hoja hii ni muhimu katika utafiti huu ambao utatambua maana mbalimbali zinazodhihirika wakati lugha ya Kibukusu na Kiswahili zinapotumika kwa pamoja katika mawanda ya dini. Hivi kwamba hali hii haitokei tu kwa sababu ya upungufu wa kiisimu wa lugha mojawapo bali hutokea kutimiza malengo maalum. Aidha, huchangia pia katika kukuza misamiati inayokubalika na inayowasilisha maana inayotekeleza majukumu yanayohusiana na miktadha ya matumizi katika Kaunti ya Bungoma.

Ayeomoni (2011) anabainisha kuwa nchi ya Nigeria ina zaidi ya lugha mia nne hamsini. Kila lugha hupewa majukumu tofauti kutegemea mawanda na shughuli. Kwa hivyo hali ya matumizi ya lugha Nigeria ni tofauti na jinsi ilivyo katika nchi nyinginezo zinazotumia lugha moja au mbili kama vile Japani na Canada mtawalia. Anaeleza kuwa kuna sera ya serikali kuhusu mawanda ya matumizi ya lugha katika katiba ya nchi ya Nigeria (1979) na sera ya kitaifa ya masuala ya elimu (1977, 1985 & 2004). Anatambua umuhimu wa kuwepo kwa majukumu teule ya kila lugha iwe ya kienyeji au ya kigeni. Lugha kwao ni njia mojawapo ya kuhimiza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

mahusiano ya kijamii, umoja wa nchi na kuhifadhi utamaduni wao. Kwa sababu za kitaifa kila mtoto anatakiwa kujifunza angalau lugha moja kwa hizi tatu, Hausa, Igbo na Yoruba. Hata hivyo, juhudi za serikali na watu binafsi za kutenga kila lugha kwa majukumu teule hali ya utohozi, kukopa, kubadili na kuchanganya msimbo bado ipo. Hali hizi hutokana na mtagusano wa lugha za kienyeji na zile za kigeni katika jamii ya wingi lugha. Wazungumzaji huweza kudhihirisha hali hizi kwa namna tofauti tofauti katika matumizi yao ya lugha. Utafiti huu unakurubiana na huu kwa namna ambavyo lugha ya Kiswahili imepewa majukumu teule ya kuwa lugha rasmi na lugha ya taifa na katiba ya nchi ya Kenya (2010). Majukumu ya lugha ya Kibukusu hayajaratibiwa ingawa ni lugha mojawapo ya kikabila nchini Kenya. Lugha hii ina umuhimu wa kuhifadhi utamaduni wa eneo hili ingawa huonekana kutumiwa pamoja na lugha ya Kiswahili katika mawanda mbalimbali. Utafiti huu utabaini namna ambavyo lugha ya Kiswahili na Kibukusu humizaniana kwa kukopa, kubadili na kuchanganya msimbo, kutohoa na kadhalika ili kutekeleza majukumu mbalimbali ya DYM katika Kaunti ya Bungoma.

Necak (2017) anapofafanua ikolojia ya Slovania karne ya ishirini, anajikita kwa mada mbili. Kwanza matumizi ya lugha moja ambayo ilikuwa lengo la wapangaji lugha wa Slovania. Walijitahidi kuunda lugha sanifu ambayo haikuhitilafiwa na Kijerumani na lugha nyinginezo kwa namna yoyote. Hali hii iliibua wazungumzaji wa Slovania wenye hadhi fulani ambao ndio walitawala kiutamaduni na kisiasa. Pili aliangazia uelekezi katika ikolojia ya lugha ambayo iliendeleza utawala wao ulioratibiwa na misingi yao ya kiisimu. Katika mazingira ya Kaunti ya Bungoma lugha za Kibukusu na Kiswahili zina hadhi tofauti kutokana na majukumu yao pamoja na miktadha ya kimatumizi. Ingawa hakuna uelekezi wa moja kwa moja na serikali kuhusu namna lugha hizi zinafaa kutumiwa uamilifu wao unabainishwa waziwazi kupitia matokeo ya utafiti huu.

Barnes (2017) katika kazi yake ya kutathmini ikolojia ya lugha kule Ireland kupitia kwa mhusika Hugo ambaye alikuzwa katika jamii ya lugha ya Ki-irish na Kijerumani. Katika kitabu hiki cha *The Speckled People* hali tatu tofauti za kiisimu zinatambuliwa. Hali ya Ki-irish inahusiana na babake Hugo, ambaye ni mzalendo anayesisitiza maendeleo ya lugha hii. Hali ya Kijerumani imehusishwa na mamake anayehusishwa na jamii ya historia ya *Nazi*. Kazi yake inachunguza mtagusano wa hali hizi mbili kwa kutambua majukumu ya ubadilishaji msimbo na pia nafasi ya lugha ya Kiingereza katika mahusiano yao. Lugha ya Kibukusu na Kiswahili miongoni mwa wakaaji wa Bungoma huonekana kutumiwa katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Ikumbukwe pia lugha ya Kiingereza kama lugha rasmi na inayotumiwa kutoa mafunzo mengi shuleni nayo huonekana kupigania nafasi ya kujiendeleza. Hali hii inaweza kuzua hofu ya kuwa matumizi ya lugha ya Kibukusu yakififia basi kuna hatari ya lugha hii kupotea. Katika utafiti wa Barnes (2017) kuna juhudi za kimaksudi za kuhifadhi lugha ya Ki-irish hata kama Hugo ako katika hali ya kutumia Ki-irish, Kijerumani na Kiingereza. Aidha, lugha hizi pia humizaniana kupitia ubadilishaji msimbo, hali ambayo tunaichunguza katika utafiti huu wa matumizi ya Kibukusu na Kiswahili katika mawanda ya dini kwa kulenga hasa DYM.

Tay (1989) anafafanua ubadilishaji na uchanganyaji msimbo kuwa mkakati wa mawasiliano hasa katika mazingira ya wingilugha. Anaendelea kusema kuwa hutumiwa kama kifaa cha kufafanua na kufasiri ili kuhimiza umoja na maelewano zaidi katika muktadha wa wingilugha. Alifanya utafiti wake kwa kuchunguza namna lugha ya Kiingereza, Mandarin, Hokkien na Toechew zinazozungumzwa Singapore zinavyotumika kwa pamoja. Mbali na tofauti za sifa za lugha hizi, mikakati inayofanana imeibuka kwa sababu ya mitagusano ya lugha katika mazingira yanayobadilika ya jamii ya wingilugha. Utafiti huu unachunguza ubadilishaji na uchanganyaji msimbo kama mikakati ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

mawasiliano ila utafiti wetu unaeleza mbinu hizi kama njia mojawapo ambapo lugha ya Kibukusu na Kiswahili humizaniana katika shughuli nzima ya kuwasiliana na hatimaye lugha hizi kuonekana kuwa hai na kutekeleza majukumu mwafaka ya kidini. Aidha, utafiti wake ulitumia nadharia za mikakati ya mawasiliano katika uchanganuzi ilhali utafiti huu unatumia nadharia ya usimamizi wa lugha.

Aidha, Makanda (2011) katika utafiti wa kuchanganua mchango wa wananchi wa kawaida katika uundaji wa sera ya lugha nchini Zimbabwe. Anaeleza kuwa watu huunda mbinu zao za kupanga, kuteua na kutumia lugha katika miktadha mbalimbali ya kijamii kwa namna ambayo inawafaa. Anaonesha namna lugha zilizotambuliwa kikatiba na zile ambazo hazijatambuliwa hutumiwa katika shughuli za kiuchumi, kisiasa na hata kijamii. Katika jamii ya kaunti ya Bungoma lugha ya Kiswahili imetambuliwa na kupewa majukumu rasmi kikatiba tofauti na lugha ya Kibukusu. Wananchi wa kaunti ya Bungoma wamejiundia upekee wao wa namna ya kutumia lugha hizi katika mawanda ya dini. Utafiti huu unalenga kubainisha nafasi ya lugha hizi katika kutekeleza majukumu ya mawasiliano ya DYM katika kaunti ya Bungoma.

Nabea (2009) anajadili kuwa nchini Kenya, sera ya lugha imetawaliwa na mitazamo inayosadifiana na hali ya kudumisha umoja wa wananchi, utaifa, utamaduni na wingi lugha. Kwa kuzingatia mtazamo wa kihistoria, sera ya lugha katika enzi ya ukoloni iliathiri pakubwa hali ya lugha kufikia kipindi cha sasa. Kwa mfano, Kiingereza na Kiswahili ni lugha ambazo zimepewa umuhimu mkubwa na serikali. Wa Thiong'o (1986) kwa upande wake anakashifu mfumo wa elimu kwa kutozingatia ufundishaji wa lugha za kiasili shuleni kwani uimarishaji wa matumizi ya lugha hizi ni rasilimali ya kimsingi kwa utamaduni na utambulisho wa kijamii. Tangu kuidhinishwa kwa mfumo wa elimu wa 8-4-4, Kiswahili ni somo linalotahiniwa na kufundishwa katika shule za msingi na upili, pamoja na vyuo. Kwa mujibu wa Mutiga (2005) ugiligili katika sera na upangaji lugha nchini Kenya umefanya lugha za kiasili kubaki nyuma katika kukua na kustawishwa. Maoni haya yalitupa msukumo wa kutathmini hali halisi ya uamilifu wa lugha ilivyo kati ya lugha ya Kibukusu na Kiswahili katika Kaunti ya Bungoma.

Shitemi (2011) na Mutiga (2005) wana msimamo kuwa, kuwepo wa takriban lugha sabini ambazo huzungumzwa na makabila mbalimbali nchini Kenya ni changamoto kwa wapangaji lugha na ni miongoni mwa sababu ambazo zinachangia kwa kiwango kikubwa, kuwepo kwa utata katika juhudi za kubuni sera thabiti na dhahiri nchini Kenya. Aidha, pana ushindani baina ya Kiingereza na Kiswahili ambao umetinga matarajio ya kutumia lugha za kiasili au za mama kama msingi wa kufundishia katika mfumo rasmi wa elimu. Katika sura ya pili ya katiba ya Kenya ya mwaka 2010 (Republic of Kenya 2010), kila raia ana haki ya kutumia lugha. Katiba ya Kenya ya 2010 inasisitiza kuhusu kutambuliwa kwa lugha zote pamoja na makundi mbalimbali ya kijamii. Hata hivyo, sera inayotambua mseto wa lugha lazima itekeleze wajibu muhimu kulingana na matarajio yanayolenga katika kudumisha demokrasia shirikishi. Katika katiba hii, mfumo wa ugatuzi umetiliwa mkazo, hasa katika sura ya kumi na moja, ambapo serikali gatuzi zinapasa kuzingatia dhima ya wingi lugha katika michakato ya kimawasiliano, lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kwamba wananchi wa mashinani wanashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo kupitia lugha wanazozielewa barabara hususan lugha za kiasili. Hili linatupa mwanya wa kutaka kutambua namna lugha ya Kibukusu inavyotumiwa katika miktadha mbalimbali zaidi isiyo rasmi kama vile ya dini katika Kaunti ya Bungoma.

Suala la matumizi ya lugha mbili au zaidi limekuwa kawaida ulimwenguni kutokana na misukumo ya usasa na utandawazi. Milroy na Muysken (1995) wanaeleza kuwa kutokana na misukumo hii imeongeza hali ya wingi lugha ulimwenguni. Wanaendelea kusema kuwa hali hii inaendelezwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

zaidi na wakati wazungumzaji wa lugha tofauti hukutana na kutangamana kijamii na kiisimu na kusababisha kuchanganya na kubadili msimbo, ukopaji, diaglossia na lugha hizi kuathiriana kimatamshi na kiothografia. Utafiti huu unachunguza nafasi ya lugha ya Kibukusu na Kiswahili katika kutimiza mahitaji ya mawasiliano kwenye mawanda yasiyo rasmi ya DYM.

Kulingana na Bamgbose (2000) alifafanua mkataba wa Barcelona katika tamko bia la Barcelona kuhusu haki kwa wanaisimu. Haki 1996 inaeleza kuwa, kila jamiilugha wana haki ya kutumia lugha kutekeleza shughuli zao zote za kiuchumi kama vile uuzaji na ununuzi wa bidhaa na huduma, kwenye benki, bima, mikataba ya kikazi na shughuli nyinginezo. Pili, lugha haitashurutishwa kutumiwa tu katika maeneo fulani pekee na kila jamiilugha inahitaji kuyaandika maelekezo haya katika lugha zao. Mtazamo huu wa Bamgbose (2000) unahimiza umuhimu wa kila lugha inayopatikana katika jamii lugha fulani. Kwa jicho hilo utafiti huu unatambua matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kibukusu katika kufanikisha shughuli mbalimbali za kijamii. Hivi kwamba lugha ya Kiswahili ina hadhi ya kuwa lugha ya kitaifa na pia rasmi na Kibukusu ni lugha ya asili ya eneo hili, ila zote zinaonekana kuwa na nafasi teule katika kufanikisha mawasiliano kwa namna moja au nyingine. Jukumu la utafiti huu ni kuweka wazi namna lugha hizi hutumiwa katika mawanda ya DYM katika Kaunti ya Bungoma.

Ferguson (1972) alieleza hali ya diaglossia kuwa uteuzi wa lugha moja kutumiwa katika miktadha rasmi na ambayo imepewa hadhi ya juu. Kuna pia lugha ya pili ambayo inatumiwa kwa miktadha ya kawaida isiyo rasmi na inayotambulika kuwa ya hadhi ya chini. Lugha hizi zimepewa majukumu rasmi na miktadha rasmi ya matumizi. Hili ni suala tata katika muktadha wa matumizi ya lugha ya Kibukusu na Kiswahili katika Kaunti ya Bungoma. Kila mzungumzaji ana upekee wake wa namna ya kutumia lugha hizi mbili. Lugha ya Kiswahili ina majukumu kama lugha ya taifa, somo la shuleni na pia lugha rasmi na Kibukusu ina nafasi yake kama lugha ya kiasili ya wakaaji wa Kaunti ya Bungoma. Lengo hasa la utafiti huu ni kuchanganua namna lugha hizi mbili hutumika katika shughuli za DYM katika Kaunti ya Bungoma.

Khadi (2015) katika utafiti wake alitambua kuwa kuna mitazamo miwili mipana ya kubadili msimbo ambayo ni ya kiisimujamii na kisarufi. Akimnukuu Riehl (2005) mtazamo wa kiisimu jamii huhusu zaidi matumizi ya lugha ilhali wa kisarufi huhusu mifumo na miundo ya lugha. Aidha, anaeleza kuwa matumizi ya lugha mbili au zaidi huhutaji umilisi katika lugha zote. Koppe na Meisel (1995) wanasisitiza kuwa umilisi wa kisarufi huhusu uwezo wa kuteua msimbo kulingana na maswala kama vile sifa za wahusika, hali za kimuktadha na mada ya mawasiliano. Wanaendelea kusema kuwa hali ya kijamii ni muhimu katika kuteua lugha ya kutumiwa katika maingiliano fulani ya kijamii. Mawazo ya wataalamu hawa yanachangia katika kutathmini hali zinazotawala uhalisia wa matumizi ya lugha ya Kibukusu na Kiswahili katika Kaunti ya Bungoma. Hivi kwamba lugha hizi hazitumiwi tu bali huteuliwa ili kuwasilisha ujumbe fulani.

Tafiti hizi zote ni miongoni mwa kazi zinazotufafanulia nafasi ya lugha katika kubainisha mawanda ya dini. Mulwale, Indede na Asiko (2022) wanaeleza kuwa ni muhimu kutambua kuwa miktadha tofauti hutumia raslimali za lugha zinazopatikana katika mazingira yake ili kufanikisha mawasiliano. Mazingira ya kazi hii yana lugha ya Kiswahili na Kibukusu. Hivyo basi kazi hii inachunguza namna ambavyo lugha hizi hutagusana ili kutekeleza majukumu ya mawanda haya ya dini ya Msambwa katika Kaunti ya Bungoma.

## MBINU ZA UTAFITI

Muundo wa kiuchanganuzi umetumiwa katika kazi hii. Utafiti huu unalenga wahusika ambao wanatumia lugha ya Kibukusu na Kiswahili katika mawanda teule ya muktadha wa DYM. Matumizi ya lugha wakati wa ibada katika dhehebu hili

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

yalilengwa kwa sababu ya imani kuwa ndilo dhehebu asili la jamii ya Wabukusu (Kuloba, 2014). Inaaminika kuwa lugha ya Kibukusu ilitumiwa katika shughuli zao.

Uchunzaji wa kushiriki moja kwa moja ulitumiwa kukusanya data katika kazi hii. Uchunzaji wa moja kwa moja ulitumika katika miktadha isiyomhitaji mtafiti kukusanya data kwa kutegemea maelezo ya watu wengine. Mbinu hii humuwezesha mtafiti kunakili matukio papo hapo yanapotokea. Wanaisimu jamii kama vile Gumperz and Hymes (1972) pamoja na Mesthrie *et al*. (2000) wanaeleza kuwa mbinu hii ni faafu kwani humuwezesha mtafiti kuwa mmojawapo wa jamii inayofanyiwa utafiti kwa namna ambavyo si mhusika moja kwa moja au si mtazamaji tu. Milroy (1980) anafafanua kuwa sifa hii huwezesha ukusanyaji wa mitindo mbalimbali ya mazungumzo asilia katika miktadha tofauti pasipo kuathiri kaida za mahusiano katika jamii. Aidha, Kwa mujibu wa Spradley (1980), mbinu hii ni faafu kwani humwezesha mtafiti kuelewa hisia na tajiriba za wahusika, pamoja na kuthibitisha data halisi ambazo huenda ziepukwe kupitia matumizi ya usaili. Uchunzaji wa kutoshiriki moja kwa moja ulizingatia mandhari na miktadha maalum ya mitagusano ya lugha, ambapo kanda ya kunasia sauti ilitumiwa kunukuu uhalisia wa matumizi ya lugha kwenye ibada za kanisa la DYM.

Matumizi ya lugha kwenye ibada yalinakiliwa kama vile kiongozi wa ibada anapowasiliana na waumini wenzake na mazungumzo kati ya waumini katika shughuli mbalimbali kama vile ubatizo, ujinaishi na ibada za kawaida.

Data iliyokusanywa kupitia kanda ya kunasa sauti ilifasiriwa na kunakiliwa. Kwa kutumia orodha ya uchunzaji yenye sifa mwafaka matumizi ya lugha ya Kibukusu na Kiswahili yalibainishwa katika shughuli mbalimbali za dhehebu hili. Flick (2008) anaeleza kuwa orodha ya uchunzaji sharti iwe na masuala machache ya kuzingatiwa ili kupata data ya kuthaminiwa. Katika utafiti huu matumizi ya lugha hizi yaliyobainishwa ni miktadha maalum ambamo uchanganyaji na ubadilishaji wa msimbo, ukopaji wa moja kwa moja, tafsiri au utohozi wa maneno kati ya Kibukusu na Kiswahili. Hivyo basi orodha ya uchunzaji ilitumiwa kubainisha nafasi ya Kibukusu na Kiswahili katika mawanda ya DYM. Data iliyopatikana ilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo

## MATOKEO YA UTAFITI NA MJADALA

Baadhi ya masuala yaliyobainika katika utafiti huu ni kwamba, matumizi ya lugha ya Kibukusu na Kiswahili katika muktadha huu wa DYM yalijitokeza katika shughuli mbalimbali za ibada kama vile; mahubiri, maombi na matangazo. Kulidhihirika mahubiri ya toba, ya kutia moyo, ya mafunzo, kuonya na kufafanua kuhusu masuala mbalimbali katika jamii. Kulikuwepo pia na maombi yenye dhima mbalimbali; ya toba, kusihi, kuomba usaidizi, kushukuru, kufukuza mapepo na roho chafu na ya kutia moyo.

Umri na mahusiano kati ya waumini yalichangia katika uteuzi wa ni lugha ipi itakayotumika na kwa muda gani. Sifa zinazobainika katika data hizi ni pamoja na kuchanganya na kubadili msimbo, utohozi, ukopaji na uandishi wa Kibukusu kwa kuzingatia Kiswahili.

Fishman (1972) anaeleza kuwa katika muktadha wa wingi lugha matumizi ya lugha hayajitokezi tu kiholela. Uteuzi wa lugha hutegemea raslimali za lugha zilizopo katika mazingira yale. Aidha, mada zinazojadiliwa, mahali na wahusika huchangia katika miundo ya lugha inayotumiwa. Katika muktadha huu wa DYM lugha hutumiwa kwa minajili mbalimbali. Hali ya kuchanganya na kubadili msimbo kati ya KS na KB linabainika katika shughuli mbalimbali za ibada kwa mfano katika maombi yafuatayo;

> *KB**: Paapa no mwana na roho mutakatifu**, ewe paapa khwanjile nenawe paapa khakhufunga nenawe.*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

*KS: Baba na mwana na roho mtakatifu, wewe baba tulianza na wewe baba tunafunga nawe.*

*KB: Paapa, omusiku* ***shetani*** *oli khungila olakhukendelelanga paapa omwene akhoya akhilwe.*

*KS: Baba muovu shetani aliye njiani ambaye anatutembelea, baba yeye mwenyewe anastahili kushindwa.*

*KB: Na khwama ano no khucha engo nakhwola nakhuloma khuli wele* ***asandi.***

*KS: Tunapotoka hapa tukienda nyumbani tukifika tunasema ni asante.*

*KB: Paapa khakaba ne bachile mu* ***makanisa mbalimbali paapa*** *wamwene* ***baongose paap****a, ne batamba ewe bapanile, olabapanila nakhuloma khuli* ***asandi.***

*KS : Baba Mungu na walioenda kwa makanisa mbalimbali baba mwenyewe waongoze baba, na waliopungukiwa baba wapiganiye, ukiwapiganiya tutasema kuwa asante.*

*KB : No okhali ewe sa ali omundu okundi ta.*

*KS: Kama si wewe hakuna mtu mwingine.*

*KB: Lola paapa sibala siicha ne* ***siayumba lakini ewe*** *wamwene* ***khuongose paapa ew****e wamwene ikula buwanga paapa khulaloma khuli* ***asandi…***

*KS: Tazama baba dunia inaenda ikiyumba lakini wewe mwenyewe tuongoze baba wewe fungua mwangaza baba tutasema kuwa asante…*

Hali ya kubadili au kuchanganya msimbo kati ya lugha hizi mbili hakuwezi kutabirika. Hutokea tu ghafla na huonekana kutimiza malengo fulani kama vile;

*Paapa no mwana na roho mutakatifu* - Baba na mwana na roho mtakatifu

Rahimi na Hematiyan (2011) anaeleza kuwa lugha ya dini hutumiwa Kukumbusha ambapo maneno hutumiwa kuyaeleza mambo ambayo yapo na yanajulikana katika muktadha huo. Usemi huu wa baba na Mwana na Roho mtakatifu umetumiwa kusisitiza kuwa maombi hutambulika kupitia imani kwa hawa watatu ambao hufanya kazi kwa pamoja.

Katika sala hili kuna matumizi ya maneno teule ambayo yamekopwa kutoka kwa KS ambayo yametumiwa katika lugha ya KB kama vile; Shetani na makanisa mbalimbali.

Kuna baadhi ya maneno ambayo ni ya KS ila yamepewa muundo wa lugha ya KB kwa mfano;

*Siayumba* – inayumba

*Asandi* – Asante

*Baongose paapa* – waongoze baba

*Khuongose paapa ewe* – tuongoze wewe baba

Katika muktadha huu hali hii inatokea pasipo mpangilio wowote maalum. Hivi kwamba Lugha hizi zinafahamika na waumini na ni njia moja wapo ya kujieleza. Matumizi ya lugha hizi kwa pamoja huenda ikamaanisha kukosa msamiati mwafaka katika lugha ya KB papo hapo basi lugha ya KS ikafidia mara moja au ni hali ya kukamilishana kwani ndizo lugha ambazo wahusika wanazifahamu na zinaeleweka katika mazingira yao.

Kulingana na Tay (1989) ambaye anafafanua ubadilishaji na uchanganyaji msimbo kuwa mkakati wa mawasiliano hasa katika mazingira ya wingilugha. Anaendelea kusema kuwa hutumiwa kama kifaa cha kufafanua na kufasiri ili kuhimiza umoja na maelewano zaidi katika muktadha wa wingilugha.

Katika mahubiri, maongezi yafuatayo yalidhihirika;

*KB: Khakhusomekho s****itabu*** *silio muundakano embiakha.*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

*KS: Wacha tusome kitabu kilichopo kwa agano jipya.*

*KB: Sitapu sienesio bali sia **Waeprania** yaani bali **Hebrews**.*

*KS: Kitabu hicho ati cha Waebrania yaani **Hebrews**.*

*KB: **Baebrania** bano ne mkhabamanyile tawe baandu bano nibo baaba batayi khwanjisha ebangeli*

*KS: Waebrania hawa kama hamjui watu hawa ndio waliokuwa wa kwanza kuanzisha bibilia.*

Matumizi ya maneno *sitabu, Waeprania na Baebrania* ni dhihirisho la ukosefu wa msamiati mwafaka unaolingana na huo katika lugha ya KB. Hata mhubiri akatumia lugha ya Kiingereza kufafanua kuwa ni kitabu cha *Hebrews.* Lugha ya KB, KS na hata Kiingereza ni muhimu katika kufafanua maana katika muktadha huu wa DYM. Lugha hizi zote zinatumika kwa wakati mmoja ili kuhakikisha kuwa msikilizaji ameelewa kinachosemwa, hali ambayo imewezeshwa na ufahamiaji wa lugha hizi katika mazingira haya.

Hali hii pia inadhihirika katika hatua ya kutoa matangazo, kwa mfano;

*KB**: Yes,** Esese esangala khanyoe endome endindi **chiripoti** chirurire **especially** khulondekhana enga kabele kamani ke khucha ebweeni wo mwami, **mheshimiwa** namupila mala sa kabukula **lusimu** ta enga napa lundi sa abukula ta, nio kaloma ali kamanyile lakini sa nanyolile **eripoti.***

*KS: Yes, mimi nafurahia wacha nitangulie niseme hivi ripoti zitoke especially kufuatana na ilivyokuwa nguvu za kwenda mbele za mheshimiwa, mheshimiwa nilimpigia na hakuchukua simu na nilipopiga tena hakuchukua na akasema kuwa amejua lakini sijapata ripoti.*

*KB: Nono aba **ndamukumbusia** ita.*

*KS: Sasa itabidi nimkumbushe sivyo?*

*KB: Mala ekindi aundi elio eli embo khuli ne busangafu bukali endalo yino khuba nende **omukeni** owichile yuno bali kechile busa khubakho nafwe **you can imagine**…*

*KS: Na lingine labda hilo la ati tuna furaha nyingi siku hii kuwa na mgeni aliyekuja huyu ati amekuja tu kuwa nasi you can imagine…*

*KB : Baandu baama aleyi mala se emanya bakendile khubikele namwe beboliile bali khendime **haraka haraka** enje asande koo.*

*KS : Watu wametoka mbali na sijui wametembea kwa miguu ama walijiambia kuwa wacha nikimbie haraka haraka niende asante.*

*KB : Manyile endi bukali bwefwe chumapili yawa wakala khube ne khwaba Esichei ne babaandi babakho enga ese nakararakho khubela naba ne **chicommitment chumapili** endayi ye **kumwes**i okwo.*

*KS : Najua kuwa wingi wetu Jumapili iliyopita labda tuwe tulikuwa Sichei na wengine waliokuwa kama mimi nilivivia kwa sababu nilikuwa na commitment Jumapili iliyopita ya mwezi huo.*

*KB : Mwachayo **asandi**, okhacha ta **please** yekumia mala khuchichakeo enga **chumapili** ng'eneyo ne bakhililwe please naloma endi khukhekhala engo tawe.*

*KS : Mlioenda asante, yule ambaye hakuenda please jikaze na twende huko kama Jumapili hiyo na wanaoshindwa please nilisema kuwa tusirudi nyumbani.*

Katika maelezo haya maneno kama vile *omukeni, Chumapili* na *kumwesi* yametumiwa badala ya mgeni, Jumapili na mwezi. Maneno haya ya KS yamechopekwa mofu zinazoambatana na KB ili

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

kuonekana kuafikiana na lugha hiyo. Ni dhahiri kuwa mzungumzaji anatumia lugha anazofahamu katika mazingira yake ili kuyafanya mawasiliano yake kuwa mepesi.

## HITIMISHO

Kutokana na kazi hii ni dhahiri kuwa ikolojia ya lugha ni muhimu katika kuyawezesha mawasiliano katika jamii lugha fulani. Hasa katika jamii ya wingilugha wazungumzaji huteua lugha bila kuzingatia muundo maalum. Matumizi ya lugha hizi hutokea kwa namna fulani ili kutimiza mahitaji ya mawasiliano ya wakati huo. Kuchanganya na kubadili msimbo, utohozi, na ukopaji hufanyika ili kutoa ufafanuzi zaidi na kuliweka swala wazi katika hali fulani. Aidha, hutumiwa pale ambapo msamiati wa haraka wa moja kwa moja hukosekana ili kufanya upashaji wa ujumbe kuwa na wepesi.

Dhana ya Ikolojia ya Lugha vilevile inakariri kuhusu dhima ya utambuzi kuhusu uhai wa lugha, malengo pamoja na miundo yake kama msingi wa ukuzaji, udumishaji na uhifadhi wa lugha. Matumizi ya lugha ya KB na KS kwa pamoja ni thibitisho la kwamba lugha hizi zipo hai katika mazingira haya ya Kaunti ya Bungoma.

## MAREJELEO


Auburger, L. (1990). “Linguistic Minority relations.” *Sociolinguistica 4*, 169-190.

Ayeomoni, M. O. (2011). Migration and Culture: Implications on Nigerian Languages. *International Journal of English and Literature*. 2 (9):195-199

Baldauf, R. B. (2005). Language Planning and Policy Research: An overview. In E. Hinkel (Ed.), *Handbook of Research in Second Language Teaching and Learning* (pp. 957–970). Mahwah, NJ: Lawrence Erlbaum Associates. https://doi.org/10.1080/14664208.2016.1129477

Baker, C. (2001). “Review of Tove Skutnabb-Kangas, Linguistic genocide in education – or worldwide diversity and human rights?” *Journal of Sociolinguistics*, 5(2), Mei 2001, 279-283.

Bamgbose, A. (2000). *Language and Exclusion: The Consequences of Language Policies in Africa.* Hamburg: Transaction Publishers.

Barnes, L. (2017). *The Speckled People: A study in Language Ecology in Ireland. A Journal of English Studies 34(1) 99-114.* https://doi.org/10.1080/10131752.2017.1333229

Barron, C., Bruce, N., & Nunan, D. (wh.) (2002). *Knowledge and Discourse. Towards an Ecology of Language.* London; Longman.

Bastardas-Boada, A. (2002). Language Planning and Language Ecology: Towards a theoretical integration, scribd.com. Http://www.scribd.com/doc/3025205/Language-Planning-and Language-Ecology-Towards-a-theoretical-integration. 10. 02. 2022.

Batibo H. M. (2005). *Language Decline and Death in Africa: Causes, Consequences and Challenges.* Clevedon: Multilingual Matters.

Brenzinger, M. (mh.) (2007). *Language Diversity Endangered*. Berlin: Mouton de Gruyter.

Ferguson, C. A. (1959). Diglossia. Word.- *Journal of the International Linguistic Association*, 15(2), 325-340.

Ferguson, C. (1968). St. Stefan of Perm and applied linguistics. In Journal of Asian Civilizations Vol. 39, No. 2, December 2016 17 Fishman, Ferguson, Gupta, (Eds.), *Language problems of developing nations.* (pp. 253-265). New York: Wiley.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147


Ferguson, C.A. (1972). *Language structure and language use*. Stanford: Stanford University Press.

Ferguson, C. (1982). Religious factors in language spread. In: Cooper, L. (Ed.): *Language spread.* Bloomington (pp. 95-106): Indiana University Press. Field, A. (2010).

Fishman, J. A. (1966). Language maintenance and language shift as a field of inquiry. In J. Fishman (Ed.), Language loyalty in the United States (p: 424-458). London: Mouton and Co.

Flick, U. (2008). *Designing Qualitative Research*. Verlag, SAGE Publication.

Gumperz, J. J., & Hymes, D. (1972). *Direction in sociolinguistics*. New York: Holt, Rinehart and Winston.

Halliday, M. A. K. (1994). *An Introduction to Functional Grammar* (2nd Ed.). London: Edward Arnold.

Hamers, J. F., & Blanc, M. H. A. (2000). *Bilingualism and Bilingualism*. Cambridge: Cambridge University Press. https://doi.org/10.1017/CBO9780511605796

Haugen, E (1953): *The Norwegian language in America: A study in bilingual behavior*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Haugen, E. (1972). The Language Ecology. Stanford University Press, Stanford.

Kaplan, R. B. & Baldauf, R. B. (1997): *Language Planning from Practice to theory.* Clevedon: Multilingual Matters.

Khadi, J. M. (2015). *A Socio-Pragmatic and Structural Analysis of Code-Switching among the Logoli Speech Community of Kangemi, Nairobi, Kenya*. Unpublished PhD dissertation, University of South Africa (UNISA). https://core.ac.uk/download/pdf/43177683.pdf.

Koppe, R., & Meisel. J. M. (1995). Code-switching in bilingual first language acquisition. *In One speaker, two languages: Cross-disciplinary perspective on code-switching,* ed. L. Milroy & P. Muysken, 276-301. Cambridge: Cambridge University Press.

Kuloba, R. W. (2014). Religion of the Ancestor(s) (Dini ya Musambwa) in East Africa: Historical and Theological Analysis. *Journal of Theology of Southern Africa vol. 149 pg. 111-125.*

Mabule, D. R. (2015). What is this? Is it code switching, code mixing or Language alternating? *Journal of Educational and Social Research, 5 (1), 339.* DOI:10.5901/jesr.2015.v5n1p339

Makanda, A.P.T. (2011). *An Investigation into the Creation of a Language Policy and subsequent Implementation in selected Domains of Life in Zimbabwe* (Unpublished PhD Thesis, Department of African languages), University Of South Africa.

Martin, P. (2007). Language Shift and Code Mixing: A case study from Northern Borneo. Australian Journal of Linguistics Vol. 25 (1) 109- 125. http://doi.org/10.1080/07268600500 113682

Mesthrie, R., Swan, J., Deumert, A. & Leap, W. L. eds. 2000. Introducing sociolinguistics. Edinburgh: Edinburgh University Press. Milroy, P. and P. Muysken., eds. 1995. *One speaker, two languages: Cross-disciplinary perspectives on code switching.* Cambridge: Cambridge University Press

Milroy, L. (1980). *Language and social networks*. Oxford: Blackwell.

Milroy, L. & Muysken, P. (1995). “Introduction: Code switching and bilingualism research.” In L. Milroy & P. Muysken (WH). *One speaker, two languages: Cross-disciplinary perspectives*


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

*on code - switching*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mulwale, B. M, Indede, F. N. & Ambuyo, B. A. (2022). Uamilifu wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Kimatumizi kwenye Kaunti ya Bungoma. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili. Jal 5 (1) 109 - 123. DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.665

Mutiga, J. (2005). "The Impact of a National Language on other indigenous Languages: The Case of Kenya," Katika DAAD. *A CrossBorders: Benefiting from Cultural Differences* (Uk. 236-249). Nairobi: DAAD Regional Office for Africa.

Nabea, W. (2009) Language policy in Kenya: Negotiation with hegemony. *The Journal of Pan African Studies, 3 (1), 121-138.*

Necak, A. L. (2017). Slovene Language Status Planning, revista de Llengua I Dret, *Journal of Language and Law, num, 67 p. 55-69.* https://dx.doi.org/10.2436/rld.i67.2017.2918

Phillipson, R. & Skutnabb-Kangas, T. (1996). "English only Waldwide or Language & Ecology?" *Tesol Quarterly*, 30(3), 429-452.

Probyn, M. (2009). Smuggling the Vernacular into the classroom and tensions in classroom codeswitching in township/rural schools in South Africa. *International Journal of Bilingual Education and Bilingualism 12 (2): 123-136.* https://doi.org/10.1080/13670050802153137

Province, N. W., & Kretzer, M. M. (2018). Language Attitude for the Use of Indigenous Language at Primary Schools in South Africa: A Case Study in Gauteng and North West Province: *The Arts and Indigenous Knowledge Systems in Modernized Africa, 245.*

Ricento, T. (2000). "Historical and Theoretical Perspectives in Language Policy and Planning." *Journal of Sociolinguistics* 4(2) uk. 196-213.

Samarin, W. (1976): *Language in religious practice*. Rowley, MA: Newbury House.

Sebba, B. (2011). Societal Bilingualism. In Wodak, R., Johnstone, B. & Kerswill, P. (Ed)., *The Sage Handbook of Sociolinguistics.* Sage Publications Ltd. https://dx.doi.org/10.4135/9781446200957.

Skutnabb-Kangas, T., & Harmon, D. (2018). Biological Diversity and Language Diversity: Parallels and Differences. In Fill, A. F. & Penz, H. (Eds.), *The Routledge of Ecolinguistics* (pp. 11-25). New York: Routledge. https://doi.org/10.4324/9781315687391-2.

Shitemi, N. L. (2011). *Kubidhaaisha na Kuwezesha Lugha Kama Sarafu ya Kiuchumi: Kielelezo cha Taaluma ya Kiswahili na Tafsiri*. Eldoret: Moi University Press.

Spradley, P. J. (1980). Participant Observation. NewYork Holt, Rinehart and Winston;Spolsky, B. (2009). Language Management, Cambridge, Cambridge University Pres

Spolsky, B. (2006): Introduction. Part II. In: Omoniyi/ Fishman (Eds.), 4-9.

Spolsky, B. (2004). *Language Policy*. Cambridge: Cambridge University Press

Stewart, W. (1968): A sociolinguistic typology for describing national multilingualism. In: Fishman, Joshua A. (Ed.): *Readings in the sociology of language*. (pp. 531-545), The Hague: Mouton,

Tay, M. W. J. (1989). Code switching and code mixing as a communicative Strategy in Multilingual Discourse. *Word Englishes vol. 8 (3): 407- 417*. https://doi.org/10.1111/j.1467- 971X.1989.tb00678.x

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1147

UNESCO, (2003). *Education in a Multilingual World*. Paris: United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization.

UNESCO, (1996). *Universal Declaration of Linguistic Rights*. Barcelona. United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization.

Vandenbussche, W. & Darqueness, J. (2011). Language and Religion as a Sociolinguistic field of study: Some Introductory notes. *Linguistica* 25 https://www.academia.edu/5053992/Language-and-religion-as-a-sociolinguistic-field-of-study-some-introductory-notes

Van Lier, L. (2000). From input to Affordance: Socia-interactive learning from an ecological perspective. In J. P. Lantolf (Ed). *Sociocultural theory and second learning* (pp. 245-259). Oxford University Press.

Wa Thiong'o, N. (1986) *Decolonising the mind-The politics of language in African literature. Nairobi:* Heinemann Kenya.

Williams, G. (1992). "*Sociolinguistics: A Sociological Critique*, London, Routledge.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.